

**SIFA NI KIGEZO CHA MSINGI KATIKA KUAJIRI WATU
WANAOTAKA KAZI SERIKALINI**

Imetolewa na Ofisi ya Rais, Tume ya Utumishi wa Umma

1. Neno sifa linaweza kuwa na tafsiri mbalimbali. Kwanza linaweza kutafsiriwa kama mafuta yanayotokana na samaki kama vile papa, nguru, dagaa n.k. na ambavyo hutumiwa kama kupaka kwenye chombo kama vile Jahazi, Ngalawa n.k ili wadudu wasitoboe na kukiharibu. Pili, sifa ni maelezo yanayoonyesha kiwango au kuthibitisha kipimo cha wastani cha hali ya kitu, jambo au mtu kama vile uzuri au ubaya, urefu au ufupi, ukubwa au udogo. Tafsiri ya pili ndiyo tutaitumia katika makala ya leo ambapo tutaangalia sifa zitakiwazo katika kuajiri serikalini.

2. Katika hali ya kawaida mtu yeyote au taasisi yoyote ile haiwezi kuajiri mtu ambaye hana sifa zinazotakiwa kufanya kazi fulani kwa sababu mtu huyo anaweza akaiharibu kazi hiyo na hivyo kuleta hasara katika taasisi husika. Kila kazi inahitaji sifa husika hasa zile zilizokubaliwa na kundi fulani. Mfano iwapo unahitaji mhandisi wa kutengeneza barabara, utaajiri mhandisi aliyesomea masuala ya barabara na kufaulu na si mhandisi aliyesomea masuala ya maji. Kumbe katika ajira yoyote ile sifa ni kigezo cha msingi kinachopaswa kuzingatiwa. Serikali imetunga na kupitisha Sheria ya Utumishi wa Umma Na. 8, 2002 ambayo pamoja na

mambo mengine inaainisha sifa ambazo zinatakiwa katika kuajiri watumishi wa umma ambao wataweza kutoa huduma zinazotarajiwa na umma.

3. Hivyo katika kushughulikia masuala ya ajira mamlaka zote za ajira/waajiri wanapaswa kuzingatia Sheria, kanuni na taratibu zinazotoa dira ya utekelezaji wa jukumu la ajira. Ili kuajiriwa katika utumishi wa umma ni lazima uwe na sifa, ujuzi na nia ya kufanya kazi kwa uadilifu. Ajira za upendeleo kama vile ukabila, udini au kutoa rushwa ili kupata ajira hairuhusiwi, ajira lazima izingatie sifa za kazi husika, mfano iwapo kuna nafasi wazi ya kazi ya Afisa Utawala, lazima ajiriwe yule aliyesomea masuala ya utawala na utumishi na kufaulu kiwango kinachotakiwa katika nafasi hiyo. Iwapo kuna sifa nyingine za ziada zinazoweza kuongeza ufanisi katika kada husika lazima zizingatiwe katika kujaza nafasi hiyo. Hii ni changamoto kwa waajiri katika utumishi wa umma kwa kuwa wanapaswa kuifahamu vizuri na kuitekeleza ipasavyo Sheria ya Utumishi wa Umma Na. 8 ya Mwaka 2002 na sheria nyingine zitakazowekwa na serikali kwa madhumuni ya kuboresha na kuelekeza ili kila taasisi ya serikali iweze kupata watumishi watakaoziwezesha taasisi hizo kutoa huduma kwa ufanisi na hivyo kuchangia katika kukuza uchumi wa nchi.

4. Tume inatoa wito kwa mamlaka za ajira/waajiri kuzingatia Sheria, kanuni na taratibu za ajira ambazo kimsingi zinabainisha sifa zinazotakiwa katika kuajiri watumishi katika utumishi wa umma.

Ndugu msomaji iwapo una maoni/ushauri au maswali tafadhali tuandikie:

Katibu,
Ofisi ya Rais, Tume ya Utumishi wa Umma,
S. L. P. 9143,
DAR – ES – SALAAM.

Au piga simu: 022 – 2126811 -4